/

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE 2/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI – MVUHA.**

1. MAHUDHURIO.

   i. Bibi. F. Mwambene – Mwenyekiti
   ii. Bibi. N. Moshi – Mjumbe
   iii. Dr. Robert Manyerere – Mjumbe
   iv. Bibi. Ester - Mwakilishi Mwanasheria – Mwalikwa
   v. Eng. Juma Chimwaga – Mwalikwa
   vi. Bibi. Grace L. Nyabange – Katibu

2. WASIOHUDHURIA.

   i. Bwana Salif Elias – Mjumbe – kwa taarifa

**1. AGENDA NA 1/11/2021 KUFUNGUA KIAKAO**

1.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao baada ya akidi kutimia, Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria. Kikao kilifunguliwa saa 5:25 asubuhi

**2. AGENDA NA 2/11/2021 KUTHIBITISHA AGENDA.**

2.1 Agenda zilizowasilishwa na kuthibitishwa zilikuwa kama ifuatavyo;

i. Kufungua kikao

ii. Kuthibitisha agenda

iii. Kupokea maombi ya Kufanya manunuzi na ujenzi kwenye Miradi ya Mendeleo na manunuzi kutoka Idara na Vitengo mbalimbali

   (a) Idara ya Mipango – Manunuzi ya kuanza ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19

   (b) TASAF - Manunuzi ya ujenzi wa Wodi ya wazazi na maabara katika Zahanati ya Mkambarani

   (c) Idara ya Afya

iv. Kupokea maombi ya Kufanya matengenezo ya magari kutoka Idara na Vitengo mbalimbali

CamScanner

v. Kufunga kikao

3. **AGENDA NA 3/11/2021 KUPOKEA MAOMBI YA KUFANYA MANUNUZI NA UJENZI KWENYE MIRADI YA MENDELEO KUTOKA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI**

(a) **IDARA YA MIPANGO**

Idara ya Mipango imewasilisha maombi ya kuridhia matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 2,060,000, 000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 103 katika shule za sekondari, kiasi cha shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 8 ya shule za sekondari na kiasi cha shilingi 220,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 11 ya shule za msingi- shikizi.

Kitengo cha Manunuzi baada ya kupokea maombi haya ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 2,060,000,000.00 fedha za UVIKO – 19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 103 katika shule za sekondari, Tshs 220,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 11 ya shule za msingi- shikizi na maombi ya Tshs 100,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 8 ya shule za sekondari

Fedha hizo zitapelekwa katika shule husika kama mchanganuo wa mgawanyo madarasa hayo kwa mujibu wa maelekezo. Aidha fedha hizo zimekuja na mwongozo wa jinsi zitakavyo simamiwa na Kamati ngazi ya Mkoa na Wilaya. Vilevile mwongozo umeekeza mafundi wa kutekeleza ujenzi huo kuwa ni kwa kutumia wakandarasi wa ndani (Domestic /Local contractors) au kwa kutumia njia ya Force Account (Taasisi itanunua vifaa na wataalamu wake) kutekeleza miradi hiyo.

Baada kupokea na kupitia mwongozo huo, Kitengo cha Manunuzi kimeshauri kwa shule ambazo zitaweza kupata wakandarasi wa ndani wapewe kazi hiyo na zile ambazo wakandarasi hawatapatikana basi kamati za usimamizi za Mashuleni zitekeleze miradi hiyo kwa Force account.

Vifaa vya viwandani kama vile saruji, bati, rangi na Tiles zinunuliwe kwa pamoja (bulk procurement) kama mwongozo unavyoelekeza.

Kitengo cha Manunuzi kimeleta manunuzi haya katika kikao hiki kwa kuridhia kuendelea na taratibu za Manunuzi na kufuata Mwongozo.

Wajumbe walipokea taarifa iliyotolewa na Katibu na kujadiliana ili kuona namna nzuri ya kufanya shughuli za ujenzi uliokusudiwa na kuridhia ushauri uliotolewa wa kutumia wakandarasi kwa shule ambazo zitapata na matumizi ya Force account kwa wale watakaushindwa kupata wakandarasi na kusisitiza kazi kufanyika kwa kufuata taratibu, sharia na kanuni za manunuzi.

CamScanner

(b) **KITENGO CHA TASAF**

**MAOMBI YA KURIDHIA MATUMIZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI 188,891,276.78 KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA MAABARA NA WODI YA WAZAZI ZAHANATI YA KIJIJI CHA MKAMBARANI**

Kitengo cha Manunuzi kilipokea maombi ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 188,891,276.78 fedha zinatoaka katika mfuko wa kupunguza umasikini (TASAF) kwa ajili ya ujenzi wa majengo mawili ya Maabara na jengo la Wazazi katika Zahanati ya Mkambarani. Fedha hizo zilipokelewa ha Halmashauri lakini shughuli za matumizi yake yatafanyika mkambarani na wanajamii ambako mradi husika unafanyika

Aidha fedha hizo zina maelekezo ambayo ni kwamba shughuli za manunuzi zote zitafanywa na Kamati ya Usimamizi lakini baada ya kuwezeshwa kwa mafunzo ikisaidiwa kwa karibu na wataalamu kutoka ngazi ya Wilaya kama Ofisi ya Manunuzi ambayo itakuwa inahakikisha shughuli za ununzi zinafanywa kwa kufuata taratibu na sheria.

Lakini pia Mhandisi wa ujenzi atahusika kwenye shughuli zote zinazohusu ujenzi kuanzia hatua ya kwanza mpaka kukamilishwa majengo ya Maabara na Wodi ya Wazazi yanayotarajiwa kujengwa kwenye zahanati Mkambarani.

Kitengo cha Manunuzi kinaleta manunuzi haya katika kikao hiki kwa kuridhia kuendelea na taratibu za Manunuzi na kufuata Miongozo.

Wajumbe baada ya kupitia na kujadiliana juu ya maombi haya walikubaliana kwav kauli moja manunuzi haya yaendelee.

(c) **IDARA YA AFYA**

**MAOMBI KUFANYA MATUMIZI KIASI CHA SHILINGI 230,000,000 KWA AJILI YA UMALIZIAJI WA MAJENGO YA MIONZI, JENGO LA KUFULIA, NA JENGO LA MAABARA KATIK HOSPITALI YA WILAYA.**

Kitengo cha Manunuzi kimepokea maombi kutoka Idara ya Afya ya kufanya manunuzi ya kutumia kiasi cha shilingi 230,000,000.00 yaliyoidhinishwa na Mkurugenzi mtendaji ya kufanya kazi ya umaliziaji wa majengo ya Mionzi, Maabara na Jengo la kufulia (Laundry).

Kitengo cha Manununuzi baada ya kupokea maombi hayo kinashauri watafutwe mafundi kwa ajili ya kufanya kazi hizi ambao watanunuliwa vifaa ili waweze kumalizia kazi zilizobakia

Wajumbe baada ya kupitia na kujadiliana juu ya maombi haya walikubaliana kwav kauli moja manunuzi haya yaendelee

CamScanner

## 4. AGENDA NA 4/11/2021 MAOMBI YA MATENGENEZO YA MAGARI KWA IDARA MBALIMBALI ZA MIPANGO, KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI, IDARA YA AFYA NA IDARA YA UTAWALA

Kitengo cha Manunuzi kimepokea maombi ya matengenezo ya magari kwa idara mbalimbali kama ifuatavyo:-

**(i) Idara ya Mipango**

Kitengo cha Manunuzi kilipokea maombi ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 7,235,400.00 fedha za kutoka kifungu cha idara ya Mipango kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya gari SM 9748 ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za idara hasa kutembelea miradi inayoendelea kutekelezwa na Halmashauri.

**(ii) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani**

Kitengo cha Manunuzi kilipokea maombi ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya gari DFPA 649. Kwamba fedha hizi zitalipwa kupitia vifungu vya fedha za mapato ya ndani

**(iii)Idara ya Afya**

Kitengo cha Manunuzi kilipokea maombi ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 8,318,092.58.00 kutoka idara ya afya kwa ajili matengenezo ya gari la wagionjwa STL 3819 fedha za kutoka kifungu cha idara ya Afya cha Development Own Source kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa huduma za dharura za wagonjwa.

**(iv)Idara ya Utawala**

Kitengo cha Manunuzi kilipokea maombi ya kuridhia kutumia kiasi cha shilingi 6,070,067.50 kwa ajili ya matengenezo ya gari SM 11962. Kwamba fedha hizi zitalipwa kupitia vifungu vya fedha za mapato ya ndani

Kitengo cha Manunuzi baaada ya kupitia maombi ya matengenezo haya kinashauri matengenezo kufanyika kwa kuwa itarahisisha shughuli za ufuatiliaji wa miradi ikizingatiwa kuwa Halmashauri inayo miradi mingi na yenye kuhitaji ufuatiliaji na utekelezaji wa haraka, Na kwamba matengenezo haya yafanyike kupitia Wakala wa huduma za mitambo na Umeme (Temesa) kwa magari yote yaliyoahinishwa hapo juu kama sheria manunuzi ya Umma inavyotaka.

CamScanner

Hivyo kitengo cha Manunuzi kimeleta manunuzi haya katika kikao hiki kwa kuridhia kuendelea na taratibu za Manunuzi na kufuata taratibu, sheria na kanuni.

**4 AGENDA NA 5/11/2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 7.50 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao

UMETHIBITISHWA

Mwenyekiti
Jina ……Frorence Mwambene……

Saini……[signature]……

Katibu
Jina ……Graca L. Nyabange……

Saini ……[signature]……

Tarehe ……30/11/2021……

CamScanner